SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.23 NO. 1 2024
DOI: 10.51984/JOHS.V23I1.2583

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/johs

# Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke katika Tamthiliya ya Kiswahili "Tamthiliya ya Alikiona kama mfano"

Ismahan Abulkasim Issa Massuod

Department of Languages and African Studies, College of Languages, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Mwanamke
Tamthiliya
Jamii
Usawiri
Alikiona

**ABSTRACT**

Makala hii inalenga kuchunguza usawiri wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya Kiswahili "Tamthiliya ya Alikiona kama mfano" Katika kufanikisha lengo hili, tulichambua usawiri wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya *Alikiona* na kuelezea uhalisia wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya *Alikiona* kwa jamii ya leo. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa usawiri wa mwanamke unajitokeza katika maeneo ya mwanamke ni uzinzi, mwanamke ni mtu wa hila na ghilba, mwanamke ni mpenda ufahari, mwanamke ni muongo, mwanamke na mmbeya, mwanamke na ujanja, mwanamke ni mtunza kumbukumbu, mwanamke ni stara, mwanamke ni mpenda kupigwa na mwanamke ni mtoa matusi. Usawiri huu wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya *Alikiona* umethibitika kuwa na uhalisia katika maisha halisi ya jamii ya Watanzania ambapo mwanamke halisi anafanana na mwanamke ambaye anatajwa katika tamthiliya. Wapo wanawake kadhaa ambao wamekuwa na sifa kama hizo za mwanamke anayetajwa katika *Alikiona*.

# تصوير ومكانة ودور المرأة في المسرحية السواحيلية "مسرحية رآها مثالاً"

اسمهان ابوالقاسم عيسي مسعود

قسم اللغات والدراسات الافريقية، كلية اللغات، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
امرأة
مسرح
مجتمع
تصوير
لقد رآها

**الملخص**

تهدف هذه المقالة الى دراسة دور المرأة في المسرح السواحيلي، وقد اخترنا مسرحية "لقد رآها " **Alikiona** للكاتب إبراهيم حسين كمثال. ومن أجل تحقيق هذا الهدف، قمنا بدراسة وتحليل صورة المرأة كما وصفت في المسرحية **Alikiona**، ووضحنا حقيقة دور المرأة في هذه المسرحية في المجتمع التنزاني المعاصر. وأظهرت نتائج البحث أن صورة المرأة آخذة في الظهور في أشكال مختلفة مثلا: الذعارة ، والتلاعب، وحب الهيبة، والكذب، والمكر، والتحجب. ولقد ثبت أن هذه الصورة لمكانة المرأة في خيال **Alikiona** حقيقي في الحياة الواقعية للمجتمع التنزاني حيث تشبه المرأة الحقيقية المرأة المذكورة في هذه الرواية حيث هناك العديد من النساء اللواتي لهن صفات مماثلة للمرأة المذكورة في مسرحية **Alikiona**.

## 1. Utangulizi

Utanzu wa tamthiliya ya Kiswahili umekuwa maarufu sana katika miaka ya hivi karibuni kutokana na kuingia uigizaji wa kibishara. Hivi sasa kumekuwa na vikundi mbalimbali ambavyo vinaigiza tamthiliya kupitia vipera vya vichekesho, majigambo… n.k.

Lengo la utafiti huu ni kuchambua usawiri wa nafasi ya mwanamke katika tamthiliya ya Alikiona iliyoandikwa na Ebrahim Hussein (1967) na kuelezea uhalisia wa usawiri wa mwanamke katika tamthiliya teule kwa jamii ya leo.

**1.2 Tamthiliya ya Kiswahili** ni utanzu ambao unapatikana katika sanaa za maonyesho na umekuwepo tangu tu pale binadamu alipoanza kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha. Sanaa za maonyesho ni utanzu mpana ambao ndani yake mna maigizo, majigambo, vichekesho, ngoma, michezo ya watoto na matambiko. Utanzu huu umekuwa ukiwasilishwa kwa njia ya ana kwa ana baina ya hadhira na fanani. Hii iliufanya utanzu huu kuwa ni tukio hai ambalo lilishirikisha hadhira na fanani katika utokeaji wake tofauti na tamthiliya andishi ambazo zinamtenga fanani na hadhira yake.

**1.2 Ebrahim Hussein** ni mwandishi nguli wa tamthiliya ya Kiswahili ambaye alizaliwa kisiwani Kilwa mnamo mwaka 1943 alikokulia na kusomea. Katika ujana wake, Hussein alikuwa

*Corresponding author:
E-mail addresses: asm.masoud@sebhau.edu.ly

*Article History : Received 18 May 2023 - Received in revised form 12 February 2024 - Accepted 16 February 2024*

mwanaharakati wa chama cha kisiasa cha Tanzania African National Union (TANU). Hussein alianza kutunga michezo ya kuigiza mwishoni mwa miaka ya 1960. Kama mwandishi, aliendelea kusomea masuala ya kazi za drama. Aliwahi kwenda Ujerumani kwa masomo ya juu kuhusu Drama katika miaka ya 1960. Kama mzawa wa Uswahilini, Hussein alibuni na kuzalisha sanaa zake kutokana na mazingira na tamaduni za Uswahilini. Mbali na Alikiona (1967), Wakati Ukuta (1967), Kinjekitile (1969), Mashetani (1971), Jogoo Kijijini (1976), Ngao ya Jadi (1976) na Arusi (1980).

**1.3 Tamthiliya ya Alikiona** iliandikwa mwaka 1967 ikiwa ni mchezo wa kusisimua kutokana na kujengwa katika taharuki kadha wa kadha ambazo zinamfanya msomaji kuwa makini anaposoma tamthiliya hiyo ili aweze kufikia katika hitimisho lake. Tamthiliya hii inaeleza juu ya Saida na mumewe aitwaye Omari ambapo tunamuona Saida akiwa na mahusiano ya kimapenzi na Abdalla ambaye si mume wake. Hata hivyo siku moja Saida alibainika kutokana na kudanganya kuwa amekwenda nyumbani kwao kumuona mama yake ambaye alidaiwa kuwa ni mgonjwa. Kumbe hakukuwa na ukweli wowote ya yeye alikwenda nyumbani kwa Abdalla na kukaa huko kwa siku kadhaa. Mara baada ya kuletwa taarifa za msiba ndipo Omari alipogundua kuwa mkewe hakuwa amekwenda nyumbani kwao kwani hata kwenye msiba hakuwepo na hapa ndipo ile methali ya Waswahili isemayo, “njia ya muongo ni fupi,” inapothibitika vizuri.

## 2. Usawiri wa Nafasi ya Mwanamke na Uhalisia wake kwa Jamii

Usawiri wa mwanamke katika kazi za fasihi ni kitu ambacho kimewavutia wataalamu mbalimbali kukitazama kutokana na fikira kuwa mwanamke anasawiriwa katika hali duni na hasi katika kazi za fasihi (Alhabib, 2012). Hali hii imetokana na mfumo dume ambao upo katika jamii ambapo mwanamke hutazamwa kama mtu tegemezi kwa mwanaume. Ebrahim Hussein katika tamthiliya ya *Alikiona* amemsawiri mwanamke katika hali mbalimbali kama ifuatavyo:

### 2.1 Mwanamke ni Mzinzi

Mwanamke kusawiriwa kama mtu mzinifu si jambo jipya kwani imekuwa hivyo
katika fasihi simulizi na fasihi andishi. Uzinifu ni kitendo cha mtu awe mume au mke kuwa na mahusiano ya kingono yasiyokuwa rasmi au halali. Hii inaonyesha kuwa mwanamke na mwanaume wote wanahusika katika uzinifu lakini mara nyingi mwanamke pekee ndiye anayetajwa kuwa ni mzinifu. Hali hii inaweza kuwa imechangiwa kutokana na hali ya kuwa mwanamke ndiye anayetakwa na mwanaume na kwa hiyo ana hiyari ya kukubali au kukataa. Hivyo, kitendo cha mwanamke kukubali ndicho ambacho kinamfanya aonekane kuwa yeye ni mzinifu na mwanaume hatajwi kama mzinifu (Ramathan, 2013). Hata hivyo, yapo mazingira ambayo yanaonyesha kuwa mwanamke ni mzinifu kama inavyojitokeza katika *Alikiona* uk. 47:

> SAIDA: Mama! Saa mbili! Haraka haraka. Bwana ondoka, mume wangu atakuja sasa hivi.
> ABDALLAH: (Anavaa shati na viatu) Bado. Hata yote ya nini?
> SAIDA: Hapana bwana, siku nyingine anakuja mapema. (Abdallah anainuka kitandani)
> SAIDA: Ah bwana tafadhali (Anamvuta mkono) Hm tafadhali fanya haraka uende.

Dondoo hili linaonyesha kuwa mwanamke ni mzinifu kutokana na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu ambaye si mume wake. Katika hali ya kawaida mwanamke ni mtu ambaye huwa anaogopa sana kuwa na uhusiano wa kingono na mwanamme mwingine halafu mume wake ajuwe kwani itahatarisha ndoa na wakati mwingine hata uhai wake. Kwa hiyo mwanamke hufanya uhusiano wa aina hiyo kuwa ni siri kubwa isijulikane kwa mtu yeyote. Inapofikia hatua mwanamke anamruhusu mwanamme kuingia ndani ya chumba na kufanya naye mapenzi katika kitanda ambacho anakitumia yeye na mme wake, ni ishara kuwa mwanamke huyo ameshazoea uzinifu.

Katika maisha halisi ya jamii wapo wanawake wengi wa aina hii ambao hudanganywa kwa vitu vidogo na hudiriki kuwaingiza mahawara ndani ya nyumba zao na kufanya nao mapenzi kitu ambacho kinahatarisha afya kwani uwezekano wa kuambukizwa magonjwa kama UKIMWI ni mkubwa.

Wataalamu wa nadharia ya Ufeministi wanaeleza kuwa hali ya mwanamke kutoka nje ya ndoa inaweza kusababishwa na mambo mengi ikiwa ni pamoja na kukosa huduma za msingi za kujikimu kutoka kwa mume wake (Koda, 2000). Hii inawafanya wanawake kuamua kutafuta mahitaji hayo nje na ndipo anapokutana na mwanamume ambaye humlaghai kuwa atampatia kila kitu.

### 2.2 Mwanamke ni Mtu wa Hila na Ghilba

Mwanamke ni kiumbe ambaye anatajwa kuwa mwenye hila na ghilba kwa mwanaume kiasi hata mwanaume akaamini kila kitu ambacho kinasemwa na mwanamke huyo (Abdalla, 2014).

Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kama kiumbe ambaye ana hila na ghilba za hali ya juu dhidi ya mwanamme. Tuone mfano katika data ifuatayo:

> ABDALLAH: Kuna watu (Anarudi mbio, anapiga mbizi chini ya mvungu wa kitanda. Kwa kuwa tendegu za kitanda zinatazama upande wa watazamaji, tunaona mvungu wa kitanda. Tunauona uso wake)
> SAIDA: (Anampokea mumewe huku anakifichaficha kitanda asitazame upande upande ule) Habari za kazini bwana?
> OMARI: Njema njema. (Anataka kukaa juu ya kiti. Akikaa juu ya kiti ataona mvungu wa kitanda)
> SAIDA: Ah usikae hapo bwana, kiti kibovu. Nilitaka kukipeleka kwa fundi lakini sikupata nafasi.
> OMARI: Kibovu?
> SAIDA: Eh kibovu. (Omari anataka kukaa juu ya mkeka.
> Akikaa juu ya mkeka ataona mvungu wa kitanda)
> SAIDA: Aah usikae juu ya mkeka (Anamkamata mkono) Mkeka mchafu.
> OMARI: Mchafu? Mbona mimi nauona safi.
> SAIDA: Mchafu sana.

Dondoo hili linaonyesha namna mwanamke alivyochorwa kama kiumbe mwenye hila kiasi cha kumzonga mumewe hata asije akamuona Abdallah aliyejificha katika mvungu wa kitanda. Saida alikuwa akifanya mapenzi na Abdallah ambaye si mumewe bali hawara ndani ya chumba anacholala yeye Saida na mume wake.

Mwanamke halisi katika jamii yupo mwenye tabia kama hii ya kuwa na uhusiano wa kingono na wanamume nje ya ndoa. Masuala ya kumficha hawara chini ya mvungu ni mambo ambayo hutokea katika maisha halisi ya kila siku ya jamii ya Kitanzania.

### 2.3 Mwanamke ni Mpenda Ufahari

Katika tamthiliya ya *Alikona* mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye anapenda mambo na maisha ya kifahari. Maisha ya kifahari

ni yale ambayo ni zaidi ya maisha ya kawaida ambayo yanamfanya mtu kuonekana kuwa yeye ni bora kuliko watu wengine. Wanawake ndio ambao wanatajwa kuwa ni wapenda ufahari na katika kuupata ufahari huwa wapo tayari kufanya jambo lolote tu lakini aishi maisha ya kifahari (Kiango, 1992). Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke amesawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda mambo ya kifahari sana. Mfano ufuatao unathibitisha hali hii:

> MAMA PILI: Habari hakuna mwenzangu ila arusi ndiyo iko wiki ijayo.
> SAIDA: Ehee, wapi? Usiniambie mmekodi Arnatoglu?
> MAMA PILI: Aaah bwana wee! Arnatoglu nini? Mama alitaka kukodi Arnatoglu. Mimi nikakataa.
> SAIDA: Kwa nini! Ndugu yangu wa mwisho mmoja tu anaolewa, kwa nini nikakodi Arnatoglu. Kina Hadija wakodi Arnatoglu na sisi vilevile? Aaah wapi? Tumejitosa, tumeichukua Diamond Jubilee.
> MAMA PILI: Na fanicha tumeagiza Nairobi.
> SAIDA: … Kama ile aliyovaa Amnei siku ya arusi yake? Ile mimi niliipenda.
> MAMA PILI: Aa veli gani ile. Veli tumeagiza Ulaya. Ulaya babu.
> SAIDA: (Anaruka ruka kwa furaha) Niambie saa!
> MAMA PILI: Nakuambia hivyo. (Anacheka). Arusi ya juzi mwenzangu-Hm Po-Mimi naliona aibu. Bwana arusi na bibi arusi kama wameokotwa, kupendeza hawakupendeza, dhiki mashaka (uk. 53-54).

Dondoo hili linaelezea namna mwanamke alivyosawiriwa kama kiumbe ambaye anapenda mambo ya kifahari. Majibizano baina ya Saida na Mama Pili yanadai kwamba harusi ya mdogo wake Mama Pili itafanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee na sio ukumbi wa Arnatoglu ambao ndio umezoeleka sana kutumiwa na watu wa kima cha chini katika maisha. Sambamba na hilo, majibizano ya Mama Pili na Saida pia yanaeleza kuwa nguo ya bibi arusi atakayovaa siku ya arusi imeagizwa kutoka Ulaya na sio kama ya Amnei iliyotengenezwa hapa hapa Tanzania.

Katika maisha halisi ya jamii wapo baadhi ya watu ambao huenda katika harusi kwa ajili tu ya kumtazama Bi. Harusi amevaaje na anafananaje na baada ya hapo ndipo maneno huzuka mtaani kama ilivyo kwa Mama Pili hapo juu. Hata hivyo, hii ni kawaida ya walimwengu na ndio saikolojia hasa ya wanawake ilivyo. Wanaufeministi wanaitetea hoja hii kwa madai kuwa mwanamke ni kiumbe ambaye anapenda vitu vizuri na pale anapoona kitu ambacho hajakifurahia lazima atasema (Ngaiza, 2002). Anaposema ndipo inakuwa ni furaha kwake lakini akibaki nacho rohoni kinamkera sana.

### 2.4 Mwanamke ni Muongo

Mwanamke kusawiriwa kama mtu muongo imejitokeza katika kazi mbalimbali za fasihi ikimuhusisha na kudanganya kitu kwa mtu kwa lengo la kufanikiwa kufanya kitu kingine ambacho si kizuri (Mangare, 2002). Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye ni muongo tena uongo usiokubalika katika jamii. Mtunzi katika uk. 51 anasema:

> SAIDA: Nataka kwenda nyumbani. (Omari anageuka kumtazama mkewe) Lakini sivyo unavyofikiria. Siku nyingi sijawaona wazee. Nipe ruhusa kesho na kesho kutwa nikawatazme wazee. Unajua siku nyingi sijawaona. Siku zile nilizokwenda, kama nilivyokuambia, mama alikuwa mgonjwa gonjwa. Utu uzima tena. (Anamkanda kimya) Kama hutaki nende basi…
> OMARI: Mke wangu mswalie mtume we, utanitoa roho. Hivyo nimekataa mimi hapa? …
> OMARI: Nenda. (Anarudi kulala). Nenda mimi radhi kabisa. Nenda mke wangu… Lini, kesho? Nenda…

Dondoo hili linamuonyesha Saida akiomba ruhusa kwa mume wake kwa ajili ya kwenda nyumbani kwa baba na mama yake kwa lengo la kuwaona wanaendeleaje maana mama yake alipatwa na maradhi. Omari alipata mashaka kama ruhusa hiyo kweli ilikuwa ni kwa ajili ya kwenda kuwaona wazazi au kulikuwa na kitu kingine. Wasiwasi wake ulichukuliwa na mkewe kama kwamba hataki kumpa ruhusa lakini Omari alijikaza na kumruhusu mkewe aende ili asijekulaumiwa kuwa alimnyima mkewe ruhusa ya kwenda kwa mumewe. Hata hivyo, Saida hakwenda kwa wazazi wake bali alikwenda kwa Abdallah ambaye ni hawara yake. Haya tunayapata pale mama yake Saida alipofariki na Saida hakuwepo msibani na wala hakujua kama mama yake ameshafariki tayari. Dondoo linasema:

> SAIDA: (Huku anachekacheka) Hodi hodi wageni hao. Jee wenyewe wapo nyumbani? (Anavua buibui. Omari amenyamaza kimya) Wanakusalimu wote, baba, mama, wote wanakupa salamu.
> OMARI: Je mama yako hajambo?
> SAIDA: Sasa mzima kabisa. Na anakusalimu sana. Aliniuliza kama kwa nini hukwenda kumtazama? Mimi nikamwambia kama kazi zimekubana sana siku hizi. Utakapopata likizo utakwenda. Nimeleta zawadi kidogo. Ndizi hizi ametoa mama. Sehemu yako.
> …
> Nimefanya nini eh? Kwa nini unanitazama namna hiyo? Sasa leo husemi? Mimi nakuuliza kama hutaki kujibu si basi. Kwani nani mwenye haja, mimi au wewe?
> …
> OMARI: Mama yako amekufa siku tatu leo. Na tumemzika juzi (Anamsukuma, Saida anapepesuka mpaka kitini, amebakia pale pale uso mikononi na huku amepiga magoti. Machozi anayataka lakini hayamjii. Amebaki anatetemeka).

Dondoo hili linaonyesha kuwa Saida hakwenda nyumbani kwao bali alikwenda mahali pengine kinyume na ruhusa aliyoomba kwa mumewe. Hapo ndipo njia ya muongo inapoonekana kuwa ni fupi kwani hakujua auweke wapi uso wake kwa aibu kubwa iliyomkuta. Baada ya kukosa pa kuuweka uso wake na asijuwe nini afanye ndipo akasema:

> SAIDA: … Nimelala nje siku tatu na mwanamume, unasikia na mwanamume. Haya kama mwanamume kweli nipige. (Anampa bakora anamshikisha mkononi, lakini Omari haichukui inaanguka chini).
> Siyo mwanamume wewe. Mkeo anachukuliwa na watu na wewe

umekaa tuu. Khanithi. Khanithi. (Anaanza kulia na kucheka pamoja. Omari anakwenda mlangoni ili atoke nje. Saida anakimbia na kujitandaza mlangoni. Ukali wote umemuondoka. Anaomba kwa sauti nyenyekevu).
OMARI: Mimi sikupigi (Kimya) (uk. 60-62).

Hapa tunaona Saida akikiri kuwa alikuwa kwa mwanamume na amelala huko kwa muda wa siku tatu. Hii ni kinyume na ruhusa ambayo aliomba kuwa anataka kwenda nyumbani kumsalimia mama yake ambaye alikuwa mgonjwa.

Katika madondoo hapo juu ambayo yanazungumzia uongo tumebaini kuwa mwanamke ni mtu ambaye anaweza kuzalisha uongo ndani ya uongo na baadaye akasema ukweli kutoka ndani ya uongo

Wanaufeministi wanakiri kwamba wanawake wa aina hiyo wapo na ni tabia na hulka ya mtu na si kwamba wanawake wote wapo hivyo (Koda, 2000). Kama ilivyo kwa baadhi ya wanamume kuwa waongo basi na wanawake nao ni hivyo lakini isitazamwe kama ni sifa ya wanawake wote katika jamii kuwa ni waongo.

### 2.5 Mwanamke ni Mmbeya

Umbeya ni hali ya kufuatilia mambo ya watu na kuyaeleza au kuyaeneza kwa umma bila ya kuulizwa na hatimaye kusababisha uhasama au kutoelewana kwa watu katika jamii. Wanawake ndio ambao wanatazamwa zaidi kuwa na sifa ya umbeya kuliko wanaume kwa sababu wanawake huwa nyumbani muda mwingi na hivyo kuwa na muda wa kutosha kufuatilia mambo yasiyowahusu (Sengo, 2009). Hata hivyo, wapo wanamme pia ambao nao hufuatilia mambo ya watu na kuyasambaza isivyohalali kwa umma. Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kama mtu mbeya ambaye anapenda kufuatilia na kusimulia kwa watu mambo ya watu wengine ambayo kimsingi hayamuhusu yeye wala hayawahusu hao ambao anawaambia. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya:

SAIDA: Ehee. Lete habari. Tunasikia tu.
MAMA PILI: Habari hakuna mwenzangu ila arusi ndiyo iko wiki ijayo.
SAIDA: Niambie sasa!
…
MAMA PILI: Kwa nini! Ndugu yangu wa mwisho mmoja tu anaolewa, kwa nini nikakodi Arnatoglu. Kina Hadija wakodi Arnatoglu na sisi vile vile? Aaah wapi? Tumejitosa, tumeichukuwa Diamond (uk. 53).

Katika dondoo hili tunaona mwanamke akisawiriwa kama kiumbe ambaye ni mbeya pale anapotoa habari za akina Hadija kuwa walikodi ukumbi fulani na hivyo yeye Mama Pili hawezi kwenda kukodi ukumbi huo.

Katika maisha halisi ya kila siku katika jamii kuna watu wa aina hii ambao muda wao mwingi huutumia kuzungumzia masuala ya watu wengine. Wanawake ndio ambao wanaonekana kuingia kwa wingi katika kundi la wambeya. Wanaufeministi wanasema kuwa mfumo dume katika jamii ndio ambao umesababisha wanawake kuwa katika kundi hili kwa sababu wanawake walio wengi wamekuwa ni akina mama wa nyumbani na hivyo muda mwingi lazima wautumie katika mambo ya umbeya (Barrett, 1988).

### 2.6 Mwanamke ni Mjanja

Ujanja ni hali ya kuwa na akili na maarifa ya ziada katika kufanya mambo kiasi cha kuonekana kuwa ni hodari. Ujanja unaweza kuwa mzuri au mbaya kulingana na aina na sababu ya kufanya ujanja huo. Mwanamke anasadikiwa kuwa ni kiumbe ambaye amepewa na Mungu maarifa ya ziada kuliko mwanaume katika baadhi ya mambo hasa yanayohusu mapenzi (Sengo, 2009). Mwanamke huonekana ni mjanja zaidi katika kuisoma saikolojia ya mwanaume na akishaijua huichezea kadiri awezavyo na atakavyo. Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kama mtu mjanja ambaye anaweza kumzuga mwanamme akazugika na kufanya kila kitu ambacho mwanamke anataka kifanyike. Mtunzi anasema:

ABDALLAH: Niambie kwanza lini utakuja?
SAIDA: Kuja wapi?
ABDALLAH: Nyumbani!
SAIDA: Je mkeo utamweka wapi?
ABDALLAH: Mke wangu kasafiri kwani we hujui?
SAIDA: Nitambwambia nini mme wangu?
ABDALLAH: Kama ungalikuwa unataka ungalitafuta njia. Wanawake mna maarifa namna kwa namna (uk. 45).

Mwanamke anaambiwa kuwa yeye ni mjanja ambaye ana mbinu na maarifa ya namna kwa namna kwamba chochote kile ambacho anataka kukifanya anaweza kufanya bila tatizo lolote.

Katika jamii wanawake wa aina hii wapo wengi tu ambao huwadanganya waume zao mambo mbalimbali na kufanya vile wanavyotaka wao.

Wanaufeministi wanaikubali hoja hii ila wanasema kuwa ni hulka ya binadamu mmoja mmoja na sio kwamba ni tabia ya wanawake wote kuwa ni wazuri wa kutumia maarifa waliyonayo katika kufanya maovu katika jamii (Skeggs, 1997). Wapo wanawake ambao wanatumia maarifa waliyonayo katika kuleta maendeleo kwa jamii yao.

### 2.7 Mwanamke ni Mtunza Kumbukumbu

Mtu mwenye kumbukumbu ni yule ambaye anatarajiwa kuwa na uwezo wa kukumbuka mambo ambayo yametokea au ameyafanya muda uliopita au mambo yaliyofanywa na watu wengine katika siku, miezi au miaka kadhaa iliyopita. Binadamu ni kiumbe ambaye anasadikiwa kuwa na uwezo wa kuweka kumbukumbu katika akili yake kwa muda mrefu ikilinganishwa na wanyama wengine. Hali ya binadamu kupoteza kumbukumbu hutokea pale umri wake unapoanza kuwa wa mtu mzima kuanzia mika 90 na kuendelea. Wapo pia ambao huanza kupoteza kumbukumbu wakiwa katika umri wa miaka 70 na 80. Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kutokuwa na kumbukumbu vizuri juu ya matendo na maneno anayozungumza. Mfano ufuataao unathibitisha kwamba:

SAIDA: Usikae hapo bwana, Nikitaka kukipeleka kwa fundi lakini sikupata nafasi.
OMARI: Kibovu?
SAIDA: Eh kibovu.
SAIDA: Kaa basi (Anampa kiti)
MAMA PILI: Nitakaa babu na roho niitue. (Omari anainuka kumpisha Mama pili. Anaona ajabu kumwona mkewe anampa kiti ‘kibovu’ mgeni. Lakini Saida kesha sahau) Jee Habari (anamwuliza Omari) Habari za kazi?
OMARI: Njema, njema, Jee nyumbani wote wazima?
MAMA PILI: Hivyo hivyo tu, hakuchi kuna kucha.
OMARI: Ndiyo maisha. (Anavaa kanzu. Anataka kutoka) (uk. 52).

Mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye hupoteza kumbukumbu mapema kabisa. Kiti ambacho Saida anampatia mgeni akae ni kile ambacho alimzuia mumewe asikalie akidai kuwa ni kibovu.

Alimzuia mumewe asikae katika kiti hicho kwa sababu kama angelikaa basi angelimuona Abdallah ambaye alikuwa amejificha chini ya mvungu

Katika jamii ambayo tunaishi mwanamke wa aina hii yupo katika jamii na hii husababishwa na uongo. Mtu anapokuwa muongo ni vigumu mno kukumbuka jana au juzi alidanganya nini na leo asikosee anapotunga uongo mwingine au anapofanya jambo ambalo linaweza kuumbua uongo wake. Hii si kwa mwanamke pekee bali hata kwa mwanamme kwamba uongo unapozidi kumbukumbu inapotea na kujikuta anaumbuka. Wanaufeministi wanakiri kuwa mwanamke kufanya mambo kwa njia za uongo humsababishia hali ya kuwa msahaulifu na kufanya makosa zaidi ya alivyotarajia.

### 2.8 Mwanamke ni Stara

Mwanamke ni stara ni nafasi ya mwanamke inayojitokeza katika kazi za fasihi ambapo mwanamke anatazamiwa kustiri maumbile yake kwa mujibu wa mafundisho ya dini na utamaduni wa jamii husika (Ramadhani, 2013). Katika tamthiliya ya *Alikiona* mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye anajisitiri kama inavyotakiwa. Kwa mfano:

> OMARI: Basi mke wangu twende hospitali. Mimi tayari. (Anamshika mkono) Haya twende.
> SAIDA: Ngoja nichukuwe buibui. (Anachukua buibui juu ya mchango) Tupite huku. (Anaonyesha njia ya uani).

Dondoo hili linathibitisha kuwa mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye anajistiri vizuri kwa kuvaa buibui. Buibui ni gauni refu na pia pana ambapo mwanamke anapovaa huonekana kuwa amejisitiri vizuri kabisa.

Hata hivyo, kutokana na maendeleo yanayoletwa na utandawazi hivi sasa baibui za wanawake zimaeanza kutengenezwa kwa namna ambayo inabana mwili tofauti na ilivyokuwa kwa baibui za zamani. Hii inamaanisha kuwa katika maisha ya siku hizi mwanamke anavaa hijabu kama geresha tu lakini si kwa lengo la kujisitiri kama mafundisho ya dini yanavyoelekeza. Hivyo, inaposemwa kuwa baibui ni gauni la heshima la stara kwa mwanamke ni vizuri kutazama ni baibui la aina gani. Wanaufeministi wa Kiislamu kwa mfano, wanasisitiza kuwa uzuri wa mwanamke upo katika kujistiri. Mwanamke ambaye anajisitiri ndiye ambaye huufanya mwili wake kuwa mzuri zaidi. Mwili wa mwanamke unatakiwa kuwa laini kwa mikono yenye kushika hivyo mwanamke anapovaa nguo ambazo zinayaficha maungo yake inakuwa ni bora zaidi katika kuufanya mwili wake kuwa laini (Were, 2012). Mwanamke ambaye anaacha wazi tu maungo ya mwili wake husababisha maungo hayo kukakamaa na kukosa ulaini unaotakiwa.

Wanaufeministi wenye msimamo mkali kwa upande wao wanaona kuwa kitendo cha mwanamke kulazimishwa kuvaa nguo gubigubi ni kumnyima uhuru wake wa kuishi vile anavyotaka kuishi. Wao wanasisitiza kwamba suala la mavazi ya mwanamke liachwe kwa mtu mwenyewe kuamua nguo ya kuvaa na asilazimishwe kuvaa nguo ya aina fulani (Mutegi, 1985). Huku ni kumnyima uhuru wa kuishi ambao kila mtu anakiwa kuishi vile atakavyo ila tu asivunje sheria na taratibu za maisha zilizowekwa katika jamii husika. Kwa mtazamo wetu tunaona kuwa si busara kumruhusu mwanamke avae nguo kwa utashi wake na hasa nguo ambazo huonyesha maungo yake. Itakumbukwa kuwa mwili wa mwanamke ni kitu ambacho kinaweza kumshawishi mwanaume hata kufikia hatua ya kubaka kiasi cha kumsababishia matatizo makubwa ya kiafya na kisaikolojia mwanamke huyo aliyebakwa.

### 2.9 Mwanamke ni Mtu wa Kupigwa

Imezoeleka katika jamii pale mwanamke anapomkosea mume wake hutarajia kupigwa ili kumfanya mwanamume aishiwe na hasira na maisha yao yaendelee kama zamani. Jambo hili limeingia katika saikolojia ya wanawake na hata baadhi ya wanaume kudhani kuwa kumpiga mwanamke ndio kumfanya asiendelee na tabia fulani ambayo amekuwa nayo (Ricard, 2000). Hii imewafanya hata baadhi ya wanawake kufanya mambo fulani wakiamini kuwa mume wake atampiga na baada ya hapo mambo yataisha na maisha yao yataendelea kama kawaida. Katika baadhi ya jamii imefikia hatua mwanamke kuamini kuwa kupingwa na mume ni kitendo cha kuonyesha upendo. Mwanamke ambaye hapigwi na mume wake hudhani kuwa hapendwi na huenda mume wake ana mwanamke mwingine nje ambaye yeye ndiye anampenda. Fikira ya mwanamke kupigwa na mume wake tumeiona katika tamthiliya ya *Alikiona* katika dondoo lifuatalo:

> SAIDA: Kwa nini hunipigi. Nipige, niue. (Anamletea kiboko, anampa mumewe) Nipige. Huwezi? Unaniogopa, ndiyo unaniogopa. (Anacheka lakini sio kicheko cha furaha lakini kicheko cha mtu aliyejiwa) Unaniogopa, ndiyo unaniogopa, kama huniogopi nipige. (Anajaribu njia nyingine)
> Nimelala nje siku tatu na mwanaume, unasikia, na mwanamume. Haya kama mwanamume kweli nipige. (Anampa bakora anamshikisha mkononi, lakini Omari haichukui inaanguka chini) (uk. 63).

Hapa tunaona mwanamke aksawiriwa kama mtu ambaye anaamini katika kupigwa kwamba ndio adhabu tosha kwa kosa alilolifanya. Katika dondoo hapo juu neno “nipige” limerudiwa mara kadhaa ikiwa ni msisitizo kwamba Saida anataka kupigwa na mumewe kwa sababu amefanya kosa la kwenda kuzini na mwanaume mwingine. Kumpiga mtu ni hatari kwa afya yake kwani anaweza kupoteza uhai au kupata tatizo la ulemavu na akaishi maisha ya shida katika kipindi chote cha maisha yake. Wanaufeministi wanasema kuwa, kumpiga mwanamke ni moja kati ya mambo ya ukatili dhidi ya jinsia.

### 2.10 Mwanamke ni Mtoa Matusi

Katika jamii wapo watu ambao hutoa matusi baada ya kuudhiwa au kwa sababu tu ni kawaida yao kutumia lugha ya matusi. Matusi ni maneno au matendo yenye kuashiria kumtusi mtu isivyo halali au isivyokubalika katika jamii. Matusi hutazamwa kama ni lugha ambayo si ya kiungwana au ambayo inakubalika katika jamii na mara nyingi hutumiwa kwa lengo la kudhalilisha au kukejeli. Matusi mengi katika jamii hutokana na viungo vya mwanadamu hususani uke wa mwanamke ndio ambao hutumika sana kama tusi kwa mtu. Katika tamthiliya ya *Alikiona* tunamuona mwanamke akisawiriwa kama mtu ambaye anatoa matusi kupitia dondoo lifuatalo:

> SAIDA: Siyo mwanamume wewe. Mkeo anachukuliwa na watu na wewe umekaa tu. Khanithi. Khanithi. (Anaanza kulia na kucheka pamoja. Omari anakwenda mlangoni ili atoke nje. Saida anakimbia na kujitandaza mlangoni. Ukali wote umemuondoka. Anaomba kwa sauti nyenyekeve) (uk. 63).

Katika dondoo hili kuna matumizi ya neno “khanithi” ambalo maana yake ni mwanamume ambaye hana uwezo wa kiuanamume. Huyo ni mwanamume ambaye uume wake hausimami kiasi cha kuweza kumwingilia mwanamke. Saida anamtukana mume wake kuwa ni khanithi kwa sababu tu amekataa kumpiga. Katika maisha halisi ni jambo la kawaida kusikia mwanamke akimtukana hata mtoto wake wa kumzaa tena matusi ya nguoni. Kwa bahati mbaya zaidi wanawake humtukana mtoto wa kumzaa kwa tusi ambalo ni kutaja

uke wa mwanamke ambaye hata yeye mtukanaji anao. Hiki ni kitu kibaya sana ambacho kinashusha thamani ya utu wa mwanamke. Ni vizuri wanajamii wakaelewa kwamba matumizi ya lugha ya matusi si kitu cha kiungwana kwani kinasababisha mtu kuonekana hana nidhamu na pia kujenga utamaduni mbaya katika jamii. Mtoto ambaye leo anatukanwa na mama yake mzazi hawezi kuishia hapo bali naye ataendelea hivyo katika maisha yake yote akiamini kuwa ni kitu cha kawaida tu mbona hata mama huwa anatukana.

## 3. Hitimisho

Kwa jumla tamthiliya ya Alikiona ina msawiri mwanamke kwa namna ambayo ina uhalisia katika maisha ya kila siku. Vipengele hivi vya usawiri wa mwanamke tulivyoviona vina uhalisia katika maisha ya kila siku ya jamii ya Watanzania na hata nje ya Tanzania. Hata hivyo, mwanamke wa siku hizi anaonekana kubadilika kidogo hususani katika masuala ya umbeya kwa sababu siku hizi wanawake wanajishughulisha. Wanawake ndio ambao wanafanya biashara ndogondogo katika masoko na mitaani na hivyo kutokuwa na muda wa kupiga umbeya. Jitihada za kuhakikisha kuwa mwanamke anapata haki ya kupata elimu inatakiwa ziendelee ili kuhakikisha kuwa mwanamke anaelimika na kufahamu mambo ya msingi ayafanye na yale ambayo si ya msingi ayaache.

## MAREJELEO

Abdallah, A. O. (2014) “Kuchunguza dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya za Shafi Adam Shafi: Mfano wa Kuli na Vuta N’kuvute,” Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

Alhabib, M. (2012). “Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarabu,” Tasinifu ya M. A Kiswahili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

Koda, B. (2000). “The Gender Dimension of Land Rights in Tanzania: Case Study of Msindo Village, Same District”, Unpublished *Ph.D Thesis,* UDSM. Dar es Salaam, Tanzania.

Ramadhani, S. K. (2013), “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee”. Tasinifu ya M.A, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Dar es Salaam, Tanzania.

1. Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AKADEMIYA.

Skeggs, B. (1997). *Formation of Class and Gender*. London: Routledge.

Were, E. (2012). “Uchunguzi wa Kilio cha Haki na Kijiba cha Roho,” Tasinifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi. Nairobi, Kenya.